



Uji

Brigid Simiyu

Catherine Groenewald

Kiswahili





Zama anajitayarisha kwenda shule.



Baba anapika uji wa kiamsha kinywa.



"Mama hutayarisha uji mzuri zaidi." Zama anasema.



Uji unampa Zama nguvu za kucheza shuleni.



Uji uko tayari.



Baba anaongeza uji maziwa kwa upendo.



"Baba, ninafikiri uji huu unahitaji sukari zaidi," Zama anasema.



"Uji wa mama una ladha kuliko wa baba," Zama anawaza.



"Baba, tafadhali naweza kupata sukari zaidi?" Zama anauliza.



Baba anamwongezea Zama 'sukari.'.



"Wu! Baba! Umeweka chumvi badala ya sukari!" Zama analalamika.



"Baba, je, mama atarudi lini nyumbani?" Zama anauliza.

You are free to download, copy, translate or adapt this story
and use the illustrations as long as you attribute in the
following way: Zimbili Dlamini and Hlengiwe Zondi Author -

Zimbili Dlamini and Hlengiwe Zondi

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Catherine Groenewald

Language - Kiswahili

Level - First words © African Storybook Initiative and

Molteno Institute 2014

Creative Commons: Attribution 3.0

Source www.africanstorybook.org



